*Kioo cha Lugha, Juz. 23(2), 331-352*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v23i2.8

# Udhihirikaji wa Utumwa katika Manamba: Uchunguzi Kifani wa Riwaya ya *Miradi Bubu ya Wazalendo*

*Angelus Mnenuka*[1]

## Ikisiri

Watu kutoka Afrika, hususan watu weusi, ni mbari iliyoathirika vibaya kutokana na maendeleo ya madola mbalimbali barani Afrika na maendeleo ya ubeberu barani Ulaya. Utumwa na ukoloni ni miongoni mwa matukio yaliyowaathiri Waafrika kiuchumi, kijamii na kisiasa, na yalimwondolea mtu mweusi hadhi ya ubinadamu wake kwa kumfanya kama mnyama au bidhaa. Madhara ya biashara ya utumwa na ukoloni bado yapo bayana. Katika Ukanda wa Afrika Mashariki, biashara ya utumwa ilikomeshwa na Waingereza katika nusu ya pili ya karne ya 19. Inaelezwa kuwa Waingereza walitokomeza biashara ya utumwa kwa misingi ya kiutu. Dai hili, ambalo lilishamiri kutokana na ongezeko la propaganda za kibeberu katika karne ya 19, linadokeza huruma ya Waingereza kutokana na udhalilishaji kwa watumwa wa Kiafrika. Hata hivyo, baadhi ya matendo waliyotendewa Waafrika wakati wa ukoloni wa Waingereza haohao, hususan katika mfumo wa manamba[2] hayatofautiani sana na yale yaliyofanyika wakati wa utumwa. Kwa kutumia kiunzi cha kinadharia cha uingiaji, tajiriba na utokaji katika utumwa kama kilivyofafanuliwa na van der Linden (2016), makala hii inalenga kujadili sura za utumwa katika mfumo wa manamba kama zinavyosawiriwa katika riwaya ya *Miradi Bubu ya Wazalendo* (Ruhumbika, 1995). Kwa kutumia kiunzi teule, imebainika kuwa michakato ya kuingia, tajiriba za utokaji katika manamba na utumwani inafanana kwa kiasi fulani. Katika riwaya teule, matendo yaliyofanywa kwa manamba yanashabihiana na yale yaliyowasibu watumwa pahala pengine duniani, hususan Afrika Mashariki na Marekani. Makala imehitimishwa kuwa mifumo yote miwili, yaani utumwa na ule wa manamba haikuzingatia utu.

## 1.0 Utangulizi

Mahusiano ya kimamlaka baina ya watu, matabaka, jamii au mataifa yanaukiliwa na mseto changamani wa masuala anuai kama vile itikadi, uchumi, nguvu za kijeshi na siasa (Mann, 1986). Hata hivyo, uwiano wa mseto huo haufanani,

[1] Profesa Mshiriki, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania
Baruapepe: amnenuka@gmail.com

[2] Pamoja na maana zingine za kijamii, hawa ni vibarua kutoka maeneo mbalimbali ya bara waliofanya kazi katika mashamba makubwa ya mkonge (taz. Sabea, 2009, 2010).

wakati mwingine, hata katika jamii moja. Matokeo yake, kumeibuka mifumo tofautitofauti ya mahusiano ya kijamii; mingine ikifanana kwa karibu na mingine ikitofautiana sana. Miongoni mwa masuala hayo ni utumwa ambapo mtu mmojammoja (au tabaka) katika jamii hutumikishwa kazi mbalimbali bila kupewa ujira stahiki. Jamii mbalimbali duniani zimekuwa na mfumo wa utumwa tangu enzi za kale kwa namna mbalimbali kutoka utumwa unaovumilika ambao wakati mwingine mtu mwenyewe anaomba kuwa mtumwa hadi utumwa wa kikatili ambapo binadamu huwindwa na kukamatwa kama mnyama kisha humilikiwa, huuzwa na kununuliwa kama bidhaa nyingine (van der Linden, 2016; Rossi, 2023). Pamoja na utumwa kuwapo katika jamii mbalimbali duniani tangu enzi za kale, kama mfumo wa maisha, bara la Afrika limeathirika zaidi kwa sababu watu wake wamekuwa wakitumiwa kama chanzo cha watumwa tangu enzi za kale katika maendeleo ya madola ya kale kama vile Misri, India na Amerika kwa karne kadhaa. Kwa mujibu wa Lane (2021), Kaskazini mwa Afrika na Kusini mwa Jangwa la Sahara, watumwa walitumiwa kama wafanyakazi, watumishi wa ndani, masuria, mafundi na katika shughuli za uziduaji wa madini. Mwanazuoni huyo anaendelea kueleza kuwa hata baada ya uvamizi wa Waarabu Kaskazini mwa Afrika katika karne ya 7 na ya 8, utumwa uliendelea. Hata hivyo, utumwa ulishamiri zaidi kuanzia miaka ya 1450 hadi miaka ya 1900 kutokana na umuhimu wake kisiasa na kiuchumi ndani na nje ya bara la Afrika (Lovejoy, 2000).

Watu weusi kutoka Afrika ni waathirika wakubwa wa utumwa na biashara ya utumwa kwa sababu hakuna mbari ya binadamu duniani iliyoondolewa sifa za kibinadamu na kutazamwa kama wanyama kama wao, ndiyo maana inaelezwa kuwa utumwa waliopitia watu weusi uliwaondolea sifa yao ya kutambuliwa kama binadamu (Ajayi, 2002). Mathalani, Douglass (2005: 6) anasisitiza akisema:

> *It may, perhaps, be fairly questioned, whether any other portion of the population of the earth could have endured the privations, sufferings and horrors of slavery, without having become more degraded in the scale of humanity than the slaves of African descent.*
>
> Labda kuna uwezekano wa kudadisi bila upendeleo wowote ikiwa kuna mbari ya watu duniani ambayo ingeweza kuvumilia ufukara, mateso na vitisho vya utumwa bila kuondolewa hadhi ya utu kama watumwa wenye asili ya Kiafrika (Tafsiri yangu).

Biashara ya utumwa inayotajwa kuwa mbaya zaidi ni ile ya Afrika Magharibi iliyoongozwa na Wazungu wakishirikiana na mawakala na wafanyabiashara kutoka ndani ya bara la Afrika, na upande wa Mashariki ikiongozwa na Waarabu wakishirikiana na wafanyabiashara wa pwani na bara. Katika biashara hizi, binadamu aliondolewa utu wake na kufanywa kama mnyama huku jamii iliyosalia ikiathiriwa kwa namna mbalimbali kisaikolojia, kiuchumi na kijamii. Dhana ya utumwa imezua mitazamo mbalimbali kutoka katika makundi tofauti. Kwa mfano, pamoja na ukatili unaofungamana na biashara hii, baadhi ya wanufaika hawakuona

ubaya wake. Pargas (2023) anaeleza kwamba baadhi ya Wazungu wa Kusini mwa Marekani walipinga madai kuwa utumwa ni udhalilishaji wa ubinadamu wakidai kuwa wao walikuwa wakiwatendea wema watumwa na walipaswa kupewa sifa kwa wema huo. Vilevile, mahusiano haya ya kitumwa yanapotazamwa katika vipindi mbalimbali vya kihistoria, yanaongeza uchangamani na utelezi katika tafsiri za utumwa ambapo wakati mwingine dhana hii huwekwa katika mawanda finyu au wigo wake hupanuliwa na kujumuisha mahusiano ambayo wengi wangeshangaa kujumuishwa katika dhana ya utumwa.

Katika muktadha wa Afrika Mashariki, kama ilivyokuwa katika maeneo mengine ya Afrika, utumwa ulikuwapo katika jamii kwa miaka mingi kama sehemu ya maisha. Biashara ya utumwa ilishika kasi katika nusu ya pili ya karne ya 19 na iliendeshwa na Waarabu wakishirikiana na wafanyabiashara wa pwani waliojulikana pia kama Waswahili na jamii za bara. Ili kujikomboa na udhalimu huu, watumwa walitumia mbinu mbalimbali. Baadhi yao walikimbia na kujificha kusikojulikana, wakatumia utoro kama njia ya kujipatia uhuru na kuanzisha "jamii huru" au "vijiji vya watumwa waliotoroka" (Iliffe, 1979: 73; Nyanto na Becker, 2025: 572). Wengine walinunua uhuru wao kwa kuwalipa wamiliki wao pesa au kwa kufanya kazi kwa kipindi fulani walichokubaliana (yaani mtumwa na mmiliki wake) ilhali baadhi yao wakiomba hifadhi katika misheni za Kikristo (Nyanto, 2019; 2024). Baadhi ya watumwa walikula viapo vya wazi mbele ya mashahidi wakionesha nia ya kupata uhuru. Viapo hivi vilitoa fursa ya kuanzishwa kwa mazungumzo kati ya watumwa na wamiliki, na serikali ya kikoloni ilitumia viapo pamoja na mashahidi na makubaliano yaliyofikiwa kama msingi wa kutoa vyeti vya uhuru wa watumwa (Nyanto na Becker, 2023).

Kuanzia mwaka 1890, Serikali ya Kijerumani katika Ujerumani ya Afrika Mashariki (baadaye Tanganyika na Tanzania Bara) ilianzisha utaratibu wa kutoa vyeti vya uhuru kwa watumwa. Vilevile, mwaka 1901, Bernhard Heinrich von Bülow, aliyekuwa Kansela wa Himaya ya Ujerumani, alitoa amri iliyowapatia watumwa haki ya kufanya kazi kwa ajili yao kwa siku mbili za wiki. Pia, amri hiyo iliwapatia watumwa haki ya kulelewa wakiwa wazee, wagonjwa, na haki ya kuuzwa kwa ridhaa yao (Nyanto, 2024). Hata hivyo, licha ya utoaji wa vyeti vya uhuru pamoja na amri ya Bernhard Bülow, utumwa uliendelea (Deutsch, 2006). Utawala wa Waingereza nchini Tanganyika ulianza mwaka 1920, na kama walivyokuwa watangulizi wao, waliazimia kukomesha utumwa. Hatimaye, Juni 1922, sheria ya kukomeshwa utumwa ilisainiwa na Kaimu Gavana wa Tanganyika, A.C. Hollis, na kutangazwa katika Gazeti la Serikali ya kikoloni ya Tanganyika (Nyanto, 2024).

Baada ya Waingereza kuazimia kutawala ukanda huo, biashara ya utumwa, na pengine, utumwa ulianza kupigwa vita. Harakati za kupinga biashara ya utumwa zikiambatana na maazimio kadha wa kadha zilifanywa huku miongoni mwa sababu zilizotajwa ni zile za kiutu. Tukio la Waingereza kupinga biashara ya utumwa kwa misingi ya kiutu limesawiriwa barabara katika riwaya ya *Uhuru wa*

*Watumwa* (Mbotela, 1959). Katika riwaya hii, kuanzia mlango wa 13 (uk. 31) hadi wa 16 (uk. 41), kunaelezwa harakati za Waingereza kuwakomboa watumwa waliokuwa wakisafirishwa kuelekea utumwani, Uarabuni. Kilongo kinachotawala ni kile cha Mwingereza mwema au Waingereza wema na Mwarabu katili kama inavyoelezwa na mwandishi baada ya watumwa kukombolewa:

> Waliambiwa wasitie hofu kwa vile walivyo mikononi mwa Mwingereza watalindwa kwa mapenzi. ... Naye atafanya kadiri ya Mungu atakavyompa uwezo kuiondoa biashara mbaya ya utumwa. ... Wenyewe hao wazee wetu mateka waliona tofauti ya Mwingereza na Mwarabu katika mema waliyofanyiwa, na ubaya waliotendwa. ... Wazungu hawakupendezewa kuona uovu huo wa hao Waarabu (Mbotela, 1959: 37-41).

Hata hivyo, inaelezwa kwamba ili kunusuru uzalishaji katika mashamba makubwa katika visiwa vya Zanzibar, Waingereza waliruhusu utumwa kuendelea (Vernet, 2013). Dai hili, na mengine kadha wa kadha, linatia wasiwasi kuhusu azma ya kuzuia biashara ya utumwa kwa misingi ya kiutu.

Ikumbukwe kuwa kabla ya ujio wa Wazungu, Waarabu waliendesha biashara ya utumwa, meno ya tembo na vipusa. Baadaye, wakoloni wa Kijerumani walifanya uvamizi na kutawala kwa mabavu. Suala hili lilikumbana na upinzani mkubwa kutoka kwa wenyeji. Vilevile, lilizua ari ya kutaka kujikomboa na ukoloni huo kama vile Vita vya Majimaji (1905-1907) katika maeneo ya kusini mwa Tanganyika (Iliffe, 1979). Baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia (1914-1919), koloni la Tanganyika likawekwa chini ya uangalizi wa Waingereza mpaka mwaka 1961 ambapo Tanganyika ilipata uhuru wake. Mwangwi wa madhila haya umejitokeza kwa namna na viwango mbalimbali katika riwaya teule. Hata hivyo, kipindi pekee cha ukoloni kinachorejelewa katika riwaya teule, ni kipindi cha karne ya 20, hususan kipindi cha utawala wa Waingereza ambapo utumwa ulikomeshwa rasmi kupitia sheria ya mwaka 1922. Licha ya kupitishwa kwa sheria, utumwa uliendelea katika maeneo kadhaa ya Tanganyika, na fursa zilizoanzishwa kukidhi matakwa ya uchumi wa kikoloni ikiwa ni pamoja na mfumo wa manamba, ziliashiria mwendelezo wa utumwa kwa namna nyingine. Makala hii inachunguza misingi ya kiutu iliyodaiwa kudhalilisha watu katika mfumo wa manamba na namna utumwa ulivyodhihirika katika utawala wa Waingereza.

### 1.1 Mfumo wa Manamba

Wakati wa ukoloni kulikuwa na maeneo ya uzalishaji, yaani migodi kama vile Lupa na Sekenke; na mashamba ya mkonge katika maeneo ya Tanga, Morogoro na Kilimanjaro; na maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya nguvukazi kama vile Ruvuma, Mbeya, Njombe, Rukwa na Kigoma. Kutokana na ukosefu wa nguvukazi uliosababishwa na wenyeji wa maeneo ya uzalishaji kutokuvutiwa na kazi zenye ujira duni, serikali za kikoloni (Wajerumani na Waingereza) zilitumia nguvukazi

kutoka maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo. Mbinu iliyotumiwa ni kuanzisha kodi ambapo ili kupata fedha za kulipa kodi hiyo na kuepuka adhabu, Waafrika walipaswa kufanya vibarua katika maeneo ya uzalishaji (Rodney, 1983). Vibarua hawa waliitwa manamba kwa sababu, badala ya kusajiliwa na kutambuliwa kwa majina yao, walitambuliwa kwa namba zao. Hata hivyo, walikuwa na kipande au kadi iliyokuwa ikibainisha jina, kiasi cha malipo na aina ya kazi walizokuwa wakizifanya (Mbilinyi, 1986).

**1.2 Utumwa katika Fasihi**

Suala la utumwa, kutokana na ukubwa na upekee wake, kama ilivyo katika masuala mengine yanayozigusa jamii mbalimbali, limejadiliwa pia katika kazi za fasihi ndani na nje ya bara la Afrika. Kwa mfano, kwa upande wa Amerika, kuna machapisho mengi kuhusu fasihi na utumwa. Yuval Taylor, na William L. Andrews na Henry L. Gates Jr., kwa mfano, wamekusanya simulizi kadhaa za watumwa na kuzichapisha. Simulizi hizo zinafafanua madhila ya utumwa. Vilevile, simulizi hizi zinaeleza tajiriba na hisia za watumwa kwa viwango mbalimbali, hususan wale waliozaliwa utumwani. Wengine waliingia utumwani wakiwa na akili timamu. Hawa wanasimulia namna walivyokamatwa, kuteswa, kusafirishwa kwa mateso, kuuzwa kama bidhaa sokoni na kuanza kuishi katika hali ya utumwa wakitendewa kama wanyama na mabwana zao mashambani au nyumbani. Simulizi hizi za watumwa zimetambuliwa kama kazi za fasihi pia (taz. Equiano, 1789; Taylor, 1999; Andrews na Gates, 2007). Fasihi ya utumwa imehakikiwa pia Amerika ya Kusini au Amerika ya Kilatini kwani idadi kubwa ya watumwa walipelekwa huko na vizazi vyao bado vipo hadi hivi sasa. Kwa mfano, Williams (1994) na Wood (2019) wamehakiki kazi za fasihi ya utumwa katika nchi za Kuba na Brazili mtawalia. Waandishi hawa wawili wanachambua kazi za fasihi zenye mrengo tofauti na ule wa Kizungu. Kwa upande wake, Williams anaeleza namna utumwa ulivyochukuliwa kijuujuu tu na waandishi wa Kizungu ilhali waandishi weusi walilijadili suala hili kwa uzito mkubwa.

Kwa upande mwingine, Wood anaeleza namna kazi za fasihi za utumwa nchini Brazili zinavyotofautiana kimaudhui na kazi nyingine za utumwa za Amerika ya Kaskazini na zile za Ulaya. Mtaalamu huyu anaeleza kuwa waandishi teule wa Brazili wanautazama utumwa na kuuhusisha na athari zake hadi hivi sasa ilhali katika nchi za Kimagharibi tatizo hili limefumbiwa macho kana kwamba halikuwahi kuwapo kama anavyosema:

> *There is reluctance within Europe's first Slave Power Nations (Portugal, Spain, Holland, Britain, and France) to see the memory of slavery as a bleeding wound. It is a wound that we have not begun to search, let alone staunch, a wound that remains open and toxic; the infection is only scabbed over* (Wood, 2019: 2).
>
> Kuna kusitasita miongoni mwa mataifa ya kwanza yaliyoendesha biashara ya utumwa (Ureno, Uhispania, Uholanzi, Uingereza na

> Ufaransa) kuona kumbukumbu ya utumwa kama jeraha la damu. Ni jeraha ambalo hatujaanza kulitafuta, achilia mbali kulitia doa, jeraha lililobaki wazi na lenye sumu; maambukizi yamefunikwa tu na kigaga (Tafsiri yangu).

Kwa hiyo, mwandishi amechambua kazi za fasihi ya utumwa nchini Brazili zinavyobainisha athari za biashara ya utumwa na utumwa wenyewe, zinavyoendelea kujitokeza katika maisha ya kila siku, suala ambalo lipo pia katika nchi nyingine lakini limefumbiwa macho. Barani Ulaya kuna simulizi za aina hii zinazowarudisha wasomaji wa fasihi katika tajiriba mbalimbali za biashara ya utumwa na utumwa wenyewe. Kwa mfano, Muñoz-Valdivieso (2020) anahakiki kazi za fasihi zilizotungwa na waandishi vizalia vya watumwa waliotokea Karibe wakieleza madhila ya biashara ya utumwa na utumwa wenyewe, wakihusisha na namna wahamiaji wanavyotazamwa nchini Uingereza. Kwa maneno mengine, wanazuoni hawa wanaeleza kuwa athari za biashara ya utumwa na utumwa bado zipo na zitaendelea kuwapo.

Si Ulaya na Amerika tu, barani Afrika kuna simulizi zinazogusia masuala ya utumwa kwa sababu ni eneo ambalo limeathiriwa sana na biashara ya utumwa kwa kuondokewa na nguvukazi kubwa kwenda mabara mengine ya Amerika, Mashariki ya Kati na Asia. Kwa upande wa Afrika Magharibi, Murphy (2012) anaeleza namna kazi za fasihi andishi za Afrika Magharibi zilivyotumia sitiari za utumwa kuibua hisia za historia iliyopita. Ingawa wakati mwingine lengo lake ni kueleza masuala yanayotokea leo lakini matumizi ya sitiari hizo yanaonesha namna biashara ya utumwa ilivyoacha kumbukumbu mbaya kwa watu wa Afrika Magharibi ambao, katika kipindi hicho, walipoteza ndugu na jamaa.

Kwa upande wa Afrika Mashariki, hali ya biashara ya utumwa na utumwa wenyewe umehakikiwa na wasanii wa fasihi andishi katika hatua mbalimbali tangu kukamatwa na kusafirishwa kutoka bara hadi pwani ya Bahari ya Hindi (watumwa wachache kutoka Afrika Mashariki walisafirishwa mpaka Bahari ya Atlantiki). Simulizi hizo zimesawiriwa katika kazi anuwai za fasihi, hususan *Uhuru wa Watumwa* (Mbotela, 1959), *Tendehogo* (Semzaba, 1984) na *Kwaheri Iselemagazi* (Mapalala, 1992). Kwa upande mwingine, kuna simulizi zilizosawiri harakati za kukomesha biashara hiyo ambapo Waingereza waliizuia si tu kwa makubaliano na Waarabu bali walifanya doria na kufanikiwa kuwaokoa baadhi ya watumwa kama inavyosawiriwa katika riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* (Mbotela, 1959).

Makala hii inahakiki namna fasihi inavyomulika utumikishwaji wa Waafrika baada ya kukomeshwa kwa biashara ya utumwa katika Ukanda wa Afrika Mashariki. Riwaya ya *Miradi Bubu ya Wazalendo* (Ruhumbika, 1995) imechambuliwa ili kuhakiki vitendo vya ukandamizaji vilivyotokea katika utawala wa kikoloni, hususan Waingereza nchini Tanganyika. Kwa maneno mengine, lengo la makala hii ni kuchambua vitendo vya utumwa katika mfumo wa ukoloni. Ni vyema kutoa muhtasari wa riwaya hii kabla ya kuanza kuichambua.

## 2.0 Riwaya ya *Miradi Bubu ya Wazalendo*

Riwaya ya *Miradi Bubu ya Wazalendo* (Ruhumbika, 1995) inasawiri historia ya Tanzania Bara kuanzia wakati wa ukoloni wa Waingereza hadi wakati Rais wa Awamu ya Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, alipong'atuka madarakani mwaka 1985. Simulizi hii inaanzia nchini Msumbiji ambapo Mzee Jabiri anaamua kuelekea Tanganyika kutafuta maisha baada ya kufiwa na ndugu zake wa karibu kutokana na maradhi yasiyojulikana. Baada ya kufika Tanganyika, Jabiri anafanya kazi ya kukata mkonge katika mashamba yaliyokuwapo mkoani Tanga akiwa pamoja na mtoto wake, Saidi. Kwa bahati mbaya, anapata ajali mbaya akiwa shambani. Kutokana huduma duni na kutojali afya za wafanyakazi, Mzee Jabiri anafariki dunia. Baadaye, Tanganyika inapata uhuru. Riwaya inaendelea kusimulia namna viongozi wa nchi wanavyotumia mamlaka zao vibaya kujinufaisha na kutimiza haja zao kwa walio chini yao.

## 3.0 Methodolojia

Ingawa riwaya hii haijadili masuala ya utumwa lakini inadokeza mahusiano ya kitumwa. Ili kutimiza lengo la makala hii, riwaya teule ilisomwa kwa makini kisha maeneo yanayoonesha mahusiano ya kitumwa yalibainishwa. Kutokana na sura changamani za utumwa, ni vyema kuwa na kiunzi kimoja cha uchambuzi ili kuepuka utelezi wa dhana ya mahusiano ya kitumwa. Kiunzi kilichoteuliwa ni kile kinachotazama utumwa katika hatua kuu tatu, yaani kuingia, tajiriba, na kutoka utumwani kama kilivyofafanuliwa na van der Linden (2016). Pamoja na tofauti na upekee wa kila aina ya utumwa (van der Linden, 2016; Pargas, 2023), si rahisi kubaini matendo ya kitumwa katika riwaya teule pekee. Hivyo, kazi mbalimbali za fasihi zinazojadili utumwa, hususan simulizi za watumwa zimerejelewa ili kusaidia kujenga hoja katika mjadala huu. Simulizi hizo zinabainisha aina za utumwa, uingiaji katika utumwa na maisha ndani ya utumwa, mtazamo wa watumwa wenyewe kuhusu namna walivyotendewa, na hatimaye namna walivyotoka utumwani. Hakika, simulizi za watumwa ni lulu kwa sababu zimeandikwa na walioshuhudia utumwa au vizalia vyao. Miongoni mwa simulizi zilizotumiwa kubaini matendo ya kitumwa ni hizi zifuatazo: *The Interesting Narrative of the Life of Olaudah Equiano Written by Himself* (Equiano, 1789); *The Narrative of the Life of Frederick Douglass: An American Slave* (Douglass, 2005), *Incidents in the Life of a Slave Girl* (Jacobs and Jacobs, 2000), '*My Mother Was Much of a Woman': Black Women, Work, and the Family under Slavery* na *The History of Mary Prince, a West Indian Slave* (Prince, 1831). Kwa upande wa Afrika Mashariki, kuna kazi kama riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* (Mbotela, 1959) na bunilizi ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* (Adam, 2007) zinazotoa simulizi hizo. Kwa ujumla, vyanzo hivi vimesaidia kubainisha matendo, mienendo na mahusiano baina ya watumwa na mabwana zao.

## 4.0 Nadharia

Kwa kuwa lengo la sura hii ni kuchambua sura mbalimbali za utumwa katika mfumo wa manamba, kiunzi cha kinadharia kinachotumiwa ni kile kinachoweza kubainisha utumwa huu unaanzia wapi, unatendekaje na unaishia wapi. Kwa hiyo, kiunzi cha kinadharia kinachoongoza uchambuzi ni kile kilichoundwa na Marcel van der Linden anayezingatia vipengele vikuu vitatu katika kuchambua kazi za shuruti au utumwa (van der Linden, 2016). Mwanazuoni huyu anapendekeza kutumia kiunzi hiki ili kuchambua utumwa au kazi za shuruti kwa kuzingatia (i) kuingia, yaani uingiaji katika mfumo wa utumwa au kazi za shuruti; (ii) tajiriba, yaani uzoefu au kupitia madhila ya mfumo wa utumwa au kazi za shuruti; na mwisho (iii) kutoka, yaani kupata uhuru tena kama binadamu wa kawaida kutoka utumwani au katika kazi za shuruti.

## 5.0 Utumwa katika Riwaya ya *Miradi Bubu ya Wazalendo*

Sehemu hii inajadili sura mbalimbali za utumwa zilizojitokeza katika riwaya teule. Kwa kuzingatia kiunzi cha kinadharia, sehemu ya kwanza, ambayo inafuata hapa chini, inachambua namna ya uingiaji katika utumwa au kazi za shuruti kama zilivyosawiriwa katika riwaya teule.

### 5.1 Uingiaji katika Utumwa

Kwa ujumla, kuna njia mbalimbali za kuingia katika utumwa au mfumo wa kazi za shuruti kama vile kuuzwa, kuzaliwa utumwani au kuingia kwa hiari (taz. van der Linden, 2016). Katika riwaya ya *Miradi Bubu ya Wazalendo,* njia pekee inayoelezwa ni kuingia utumwani au katika kazi za shuruti ni ile ya hiari. Hata hivyo, kwa mujibu wa van der Linden (2016), katika utumwa wa aina hii, hiari hiyo huwekwa katika mazingira ambayo mwathirika hana chaguo lingine, hususan baada ya kulazimishwa kulipa kodi kwa fedha taslimu. Kwa hiyo, ni kama vile mazingira ya ushurutishaji yameandaliwa kimkakati ili chaguo pekee linalowezekana liwe kuingia utumwani kwa hiari. Wengine waliingia katika mfumo wa manamba kutokana na matatizo yaliyowakabili maeneo waliyotokea. Kwa mfano, katika riwaya ya *Miradi Bubu ya Wazalendo*, inaelezwa kuwa mzee Jabiri aliondoka kwao Msumbiji kutokana na kufiwa mfululizo na jamaa zake wa karibu. Vivyo hivyo, inaelezwa pia Mnyapara Munubi aliingia katika mfumo wa manamba baada ya kutoroka kwao akikimbia adhabu kwa sababu ya kumpiga karani wa Kireno, "... ukweli ulikuwa ni kwamba Mnyapara Munubi naye ni shida ndizo zilizomfikisha hapo kwa Bwana Tumbo Tumbo..." (Ruhumbika, 1995: 23). Halikadhalika, Mnyapara Munubi alitoroka tena usiku mmoja kwenda kufanya kazi kwa tajiri mwingine anayeitwa Joji karibu na mji wa Morogoro. Kwa ujumla, hiari inayoelezwa hapa haitokani tu na hali ngumu, wakati mwingine sehemu ya manamba ilikuwa sehemu salama ya kukimbilia na kupokelewa kirahisi kwa sababu ya uhitaji mkubwa wa nguvukazi. Sehemu inayofuata inajadili matendo mbalimbali waliyofanyiwa manamba ambayo yanahusishwa na yale ya kitumwa.

## 5.2 Tajiriba za Utumwa katika Manamba

Sehemu hii inachambua tajiriba mbalimbali walizopitia manamba. Tajiriba hizi zinasaidia kubaini madhila yaliyowakumba manamba ambayo yanalinganishwa na yale yaliyopitiwa na watumwa. Lengo kuu la ulinganishi huu ni kubaini iwapo kuna tofauti za msingi baina ya watumwa na manamba. Tajiriba zimejitokeza katika maeneo yafuatayo: ufanyaji wa kazi ngumu na unyanyasaji wa watoto, udhalilishaji unaodhihirika katika utwezaji, adhabu ya viboko, lishe duni na maziko yasiyozingatia heshima za kiutu. Tajiriba za utumwa zinadhihirika pia kupitia unyonyaji na kazi za kiimla.

### 5.2.1 Ufanyaji wa Kazi Ngumu na Unyanyasaji wa Watoto

Suala la watoto kufanya kazi za kawaida, kamwe halitazamwi kama utumwa au unyanyasaji wa watoto. Lakini watoto wanapofanya kazi ambazo zinapaswa kufanywa na watu wazima, ndipo suala la unyanyasaji linapoingia. Kwa mfano, katika riwaya teule, Saidi, mtoto mwenye takribani miaka 10, alikuwa akikata mkonge na kulipwa ujira kama watu wazima. Katika hali ya kawaida, kazi ya kukata mkonge si kazi inayofanywa na mtoto wa chini ya miaka 15. Umri wake haukuwa wa kufanya kazi ngumu kama kukata mkonge, ndiyo maana utendajikazi wake uliwashangaza wengi kama inavyoelezwa katika riwaya:

> Lakini kabla hata miezi mitatu kupita, Saidi akawashangaza manamba wote hapo shambani, hadi baba yake mzazi, kwa kumudu naye kukata mkonge na kujaza mita kwa kutwa! (Ruhumbika, 1995: 5).

Mshangao huo unadokeza kuwa, katika shamba husika na mashamba ya jirani, hakukuwa na watoto kama Saidi waliokuwa wakifanya kazi hiyo. Kwa kuwa utu wa mtu mweusi haukupewa hadhi kubwa, yumkini ndiyo maana watoto wadogo waliruhusiwa si tu kufanya kazi, bali kazi hatarishi zilizopaswa kufanywa na watu wazima. Bila shaka, kama misingi ya kiutu ingelizingatiwa basi kungelikuwa na namna ya kumuwezesha Saidi kufanya kazi nyepesi zaidi kulingana na umri wake ili walau apate ujira ambao ungemuwezesha kupata posho ya chakula kama manamba wengine.

Akijadili kuhusu utumikishwaji wa watumwa wadogo, Prince (1831) anadai kuwa alikuwa na majukumu ya kuwakamua maziwa ng’ombe kumi na mmoja, kisha kuwatunza watoto na kufanya kazi zingine za nyumbani. Vilevile, katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad*, Kijakazi, mtoto aliyezaliwa na mtumwa anatumikishwa kazi mbalimbali bila mapumziko kama inavyoelezwa na mwandishi:

> Kazi za Kijakazi zilikuwa nenda-rudi, mara afanye hili mara afanye lile, mara aende huko mara aende kule, mara achukue hiki mara achukue kile, kutwa kucha. Mara nyingi baada ya kuifanya kazi hurejeshwa kuifanya kazi hiyo mara ya pili. ... Kabla ya kutimiza amri aliyopewa mwanzo, mara Bibi Maimuna, mke wa Bwana Malik, naye

> hutoa yake, "Kijakazi! Hebu kanitekee maji hapo kisimani nataka kuja kukoga, ma'na'ke n'najihisi n'nanuka jasho."
>
> "Maji nishateka, Bibi, lakini nitakwenda kuteka tena."
>
> "Unakwenda wapi tena? Unafikiri huko kisimani kuna maji ya kuchezea?" (Adam, 2007: 1)

Kwa kweli ni kawaida kwa watumwa hata wale wenye umri mdogo kutumikishwa kazi nyingi bila kupumzika. Yumkini sababu kubwa ni kuwaona wao si binadamu wa kawaida, ikizingatiwa kuwa, katika miktadha yote miwili, watumwa hawa walikuwa watu weusi huku mabwana zao wakiwa Wazungu na wenye asili ya Kiarabu.

### 5.2.2 Udhalilishaji na Utwezwaji

Kudhalilisha ni kitendo cha kumwondolea mtu heshima ya utu anayostahili kama binadamu. Kitendo cha kudhalilisha kinaweza kufanywa kwa maneno au kwa matendo. Kwa hiyo, matusi, kejeli, dharau, kumpiga au kumdhihaki mtu ni mifano michache ya udhalilishaji. Katika riwaya teule, vitendo vya udhalilishaji vimejitokeza kwa sura mbalimbali, hususan vikielekezwa kwa manamba ambao walikuwa kwenye hadhi na mazingira ya kitumwa. Si rahisi kwa udhalilishaji wa aina hiyo kutokea kwa kibarua wa kawaida katika jamii. Miongoni mwa vitendo vya udhalilishaji katika riwaya teule ni matendo ya utwezaji, kufanyishwa kazi zisizo na staha na kufanyiwa matendo yanayokiuka utu wa binadamu.

Baadhi ya matendo waliyofanyiwa watumishi wa ndani, pamoja na ujira mdogo waliopata, kwa hakika, yalikuwa ya kiudhalilishaji kwa sababu katika hali ya kawaida hayapaswi kufanywa. Baadhi ya matukio yaliyobainishwa katika riwaya teule ni kutoa huduma kwa mtu mzima asiye na tatizo la kiafya. Kwa mfano, katika riwaya ya *Miradi Bubu ya Wazalendo,* mhusika Tumbo Tumbo anaelezwa kuwa mlafi na, kutokana na ulafi wake ni mnene kiasi kwamba anahitaji maboi wake waongozane naye chooni ili kumsafisha:

> "Na kila alipokwenda haja kubwa, mmoja wa hao maboi wake ilikuwa hana budi kuandamana naye humo chooni na anapomaliza kujinyea ovyoovyo uvundo wa mavimbizi ya ulafi wake wa kula kama fisi huyo boi anamtawadha hayo mavi yake!" (uk. 14).

Hao maboi wanaonekana kufanya kazi zisizo na staha kwa sababu aliyefanyiwa hakuwachukulia maboi hao kama binadamu kamili. Inaelezwa kuwa familia ya Mzungu huyo ilikuwa Ulaya. Yumkini kitendo hicho alichokuwa akifanyiwa Tanganyika na maboi kisingewezekana kufanywa katika nchi yake ya Ulaya kwa sababu ya kuhusishwa na hisia za utumwa. Matukio kama haya yanayotia kinyaa ni kawaida kufanywa na watumwa kwa sababu watumwa hawaonekani kama binadamu wa kawaida.

**5.2.3 Utolewaji wa Adhabu ya Viboko Hadharani**

Kwa mujibu wa Chinyere (2024), adhabu ya viboko na adhabu nyingine zinazoendana na hiyo kama vile kuhasiwa, kutengwa na jamii, kudhuriwa au kuuawa si ngeni hapa duniani. Adhabu za aina hii zilitumiwa katika jamii nyingi hapo zamani kama njia ya kukomesha mienendo isiyofaa katika jamii (Chinyere, 2024). Baadaye, adhabu hizi zilionekana kuwa za kikatili na zenye kudhalilisha utu wa mtu (Bamgbose, 2015). Ndiyo maana katika hali ya kawaida, haitarajiwi mfanyakazi au kibarua kupigwa viboko kama adhabu baada ya kutenda kosa kwani kuna adhabu nyingi mbadala zinazoweza kutolewa. Hata jamii zinazoendelea kutoa adhabu hiyo kwa watu wazima, hufanya hivyo kwa wale wanaotenda makosa makubwa sana ambayo hayatarajiwi kufanywa na mtu yeyote katika jamii (Chinyere, 2024). Baadhi ya makosa ambayo hayavumiliki katika baadhi ya jamii ni kijana kumpiga mzazi wake, mtu mzima kujihusisha kimapenzi na mtoto mdogo, tuhuma za kishirikina na matukio makubwa ya kiudhalilishaji kwa mwenza.

Katika riwaya teule, adhabu hii ilikuwa ya kawaida kutolewa kwa manamba, vijana na wazee. Inaelezwa kuwa kulikuwa na eneo maalumu la kutolea adhabu ya viboko. Adhabu iliamriwa na (Mzungu) mmiliki wa shamba na mnyapara aliitoa kwa maelekezo ya mmiliki huyo kama inavyoelezwa hapa chini:

> Kwenye ofisi hiyo ya manamba ndipo pia manamba wenye makosa walipokwenda kupigwa viboko na jambazi katili Mnyapara Munubi, akiwa amesimamiwa na Bwana Tumbo Tumbo mwenyewe (uk. 12).

Wakati mwingine, adhabu hiyo ilikuwa kubwa kupita kiasi kwani ilitolewa na mtu mwenye nguvu na kusababisha maumivu makubwa kwa manamba kama inavyoelezwa katika riwaya ya *Miradi Bubu ya Wazalendo*:

> ... ilikuwa ni adhabu yenye nia ya kuua mtu hasa! Kwanza huyo maskini alivuliwa nguo zake zote, halafu akawekewa matakoni kitambaa cha chumvi, na hapo kwenye uchi wa matako yake uliolowanishwa kwa kitambaa cha chumvi ndipo akapigwa hivyo viboko! Na kwa kiboko hasa cha mjeledi wa ngozi ya kiboko. Na viboko visivyopungua ishirini na nne na kuendelea (uk. 27).

Ili kudhihirisha udhalilishaji, inaelezwa kwamba adhabu ya viboko ilitolewa hadharani ili liwe fundisho kwa wengine. Vilevile, adhabu hiyo ilitolewa kwa ufanisi mkubwa ili kutisha wengine wasifanye makosa kama inavyoelezwa hapa chini:

> Mnyapara Munubi kujikuta amezungukwa na manamba wenzake wa kambi nzima huku ameshikilia mlingoti wa kiboko na hapo chini amelala huyo kizee wa watu na mvi zake akiwa uchi kabisa kabisa na amewekewa hicho kitambaa cha maji-chumvi matakoni, ili viboko atakavyompiga vimwingie mwilini sawasawa... Kitu alichotambua tu ni kwamba alikuwa ameachia kupiga na kuna mtu anammwagia huyo

> mzee hapo chini ndoo ya maji kichwani na hapo matakoni alipompiga ni damu tupu! (uk. 28).

Inawezekana manamba wengi walipata matatizo ya kisaikolojia kutokana na adhabu hii kutolewa bila kujali umri ambapo watu wazima walipewa adhabu za udhalilishaji mbele ya watoto wao au majirani wadogo. Adhabu ya kupigwa viboko mbele ya watu wengine imeelezwa karibu katika kila simulizi ya watumwa ambapo baadhi ya watumwa walipewa adhabu hii wakiwa katika hali ya utupu. Kwa mfano, simulizi ya Mary Prince, Fredrick Douglass na ile ya Herriet Jacobs zinadokeza matukio mengi ya watumwa kupigwa viboko au wakishuhudia wenzao wakipewa adhabu hiyo wakati mwingine hata kwa makosa ya kusingiziwa. Kwa mfano, Douglass (2005: 28) anasema:

> *I have seen Colonel Lloyd make old Barney, a man between fifty and sixty years of age, uncover his bald head, kneel down upon the cold, damp ground, and receive upon his naked and toil-worn shoulders more than thirty lashes at the time.*
>
> Nimeshuhudia Kanali Lloyd akimvua kofia mzee Barney, mtu mwenye takribani miaka hamsini au sitini hivi, na kumpigisha magoti kwenye ardhi ya baridi yenye unyevunyevu, kisha kumpiga mijeledi zaidi ya thelathini kwa wakati mmoja kwenye mabega yake yaliyochoka na yenye majeraha mengi (Tafsiri yangu).

Licha ya kuumiza na kuacha makovu makubwa kwa watumwa, adhabu hii ililenga kudhalilisha utu wa mtu ili wasijione kuwa wao ni watu kama wengine, badala yake, wakubaliane na hali hiyo ya utumwa. Ndivyo ilivyokuwa kwa manamba kwamba kwa kupewa adhabu ya viboko, ilidhihirisha kuwa utu wao haukuwa sawa na mabwana zao Wazungu kwa misingi ileile iliyohalalisha na kuendeleza utumwa.

### 5.2.5 Maziko Yasiyozingatia Heshima za Kiutu

Kifo ni miongoni mwa matukio yanayoacha majonzi kwa wafiwa. Kutokana na simanzi, jamii mbalimbali zimekuwa na miviga anuai ya kuhifadhi au kuteketeza wafu ili kuonesha ukaribu wao na kuwaweka marehemu katika kumbukumbu nzuri ya kijamii (Shimane, 2018). Miongoni mwa dhima mbalimbali za miviga ya mazishi, pamoja na kukuza masuala ya kiimani kuhusu kifo na maisha baada ya kifo ni kuwasaidia wafiwa kuikubali hali na kuendana na mazingira mapya baada ya kumpoteza ndugu yao. Ndiyo maana, miviga (ibada) kwa mujibu wa imani ya jamii pamoja na ushiriki wa watu huchangia kuwaliwaza wafiwa (O'Rourke, Spitzberg na Hannawa, 2011; Hoy, 2013). Maana yake, mazishi yanayokiuka miviga ya kijamii huacha simanzi kubwa kwa wafiwa.

Inaelezwa kuwa manamba waliofariki dunia hawakuwa wakizikwa kwa heshima za kiutu wala kuzingatia miviga ya jamii husika. Kutotilia maanani mazishi ya manamba kulionesha dhahiri thamani ndogo ya manamba machoni pa

Wazungu, yaani hawakuwaona Waafrika kama binadamu wa kawaida wenye hisia na maumivu ya kufiwa. Kwa mfano, inaelezwa kuwa manamba waliofariki dunia walikuwa wakitupwa katika dimbwi la kinyesi; ndivyo alivyozikwa Mzee Jabiri.

> Kwenye hayo mavi ndimo usiku huo Mnyapara Munubi na huyo mtoto mchanga wa marehemu, Saidi, walimofikia kutupa maiti ya Mzee Jabiri, wamesimamiwa na Bwana Tumbo Tumbo, akiwahimiza kwa kuwafokea, "Tupa chafu ya maiti yenu haraka, upesi!" (uk. 20).

Kifo cha mtu mzima kina uzito kwani anapaswa kuhifadhiwa kwa miviga stahiki si kwa sababu ya heshima za kiutu pekee bali kwa misingi ya kiimani ambapo katika jamii nyingi za Kiafrika, kutokumhifadhi vyema marehemu au kukiuka baadhi ya miviga kunaweza kusababisha majanga katika kaya na jamii kwa ujumla (Mbiti, 1975; Alembi, 2002). Simulizi mbalimbali za watumwa zimesheheni matukio ya aina hii ambapo watumwa waliofariki hawakufanyiwa miviga inayotakiwa kiasi kwamba wakati mwingine watumwa wenzao walilazimika kufanya miviga yao usiku kwa sababu hawakuruhusiwa kufanya hivyo mchana. Suala hili lilitia uchungu zaidi kwa sababu utwezaji huo hauishii tu kwa marehemu aliyekuwa akizikwa wakati huo bali na wengine walitambua kile ambacho wangefanyiwa wao wenyewe baada ya kufariki dunia. Kwa mfano, Henry Bibb anaeleza namna ambavyo maziko ya watumwa yalivyokosa thamani. "*As to the burial of slaves, but very little more care is taken of their dead bodies than if they were dumb beasts*" (Bibb, 2001: 118). "Kwa upande wa mazishi ya watumwa, hakukuwapo hali ya kujali kama ilikuwa miili ya binadamu bali ilichukuliwa kama miili ya wanyama wengine tu" (Tafsiri yangu). Vilevile, Herriet Jacobs anasimulia kuhusu watumwa wawili waliouawa kwa kupigwa na rungu kwa kosa la kula nyama ya nguruwe na kunywa divai. Miili ya watumwa hao iliwekwa katika majeneza yaliyotengenezwa ovyoovyo na kuzikwa kama mbwa (Jacobs na Jacobs, 2000: 52). Kwa hiyo, suala la kutokujali miili ya manamba linafanana kabisa na yale yaliyokuwa yakitokea wakati wa utumwa.

Kwa nini hasa watu hudhalilisha wengine? Kwa mujibu wa Sharkey (1992), udhalilishaji hufanywa kwa malengo maalumu, yaani anayedhalilisha pamoja na mbinu anazozitumia hulenga kutimiza lengo fulani. Miongoni mwa sababu zinazomfanya mtu mmoja amdhalilishe mwingine ni kudhihirisha na kudumisha mamlaka pamoja na kuridhika au kufurahia mamlaka husika. Vilevile, kudhalilisha kunalenga kupinga au kudhibiti mwenendo fulani usiofaa, kujamiisha katika utamaduni, na kudumisha umoja (Gross na Stone, 1964; Sharkey, 1992). Katika riwaya teule, udhalilishaji umefanywa kwa malengo ya kudumisha mamlaka na kudhihirisha pengo kubwa la kihadhi baina ya mabwana na manamba. Tofauti kubwa hapa ni majina tu kuwa Tanganyika waliitwa "manamba" na kwingine waliitwa "watumwa" lakini hakukuwa na tofauti za namna walivyotendewa na mabwana zao. Ndiyo maana inasisitizwa kuwa manamba ilikuwa aina mojawapo ya utumwa.

**5.2.6 Huduma Duni za Lishe na Afya**

Linapokuja suala la afya na chakula, binadamu wote bila kujali tabaka, rangi, cheo au nafasi kijamii wanapaswa kupata huduma hizo kwa uhakika kwani ni huduma pekee zinazomhakikishia binadamu ustawi wa kijamii na kiuchumi. Mazingira ya manamba na ufanyaji kazi za uhamaji kwa kiasi kikubwa yaliwapora haki mbalimbali vibarua hao. Miongoni mwa sababu zilizochoea kupokwa haki hizo ni kuishi mbali na nyumbani tena katika mazingira hatarishi kwa afya na uhai wao. Kutokana na huduma duni sana za kiafya, baadhi ya wafanyakazi walifariki dunia. Muktadha huu unadokeza kuwa hata wale waliofanikiwa kurudi kwao, walidhoofika kiafya kutokana na lishe duni, kazi ngumu na adhabu za kudhalilisha. Inaelezwa vilevile, miongoni mwa adhabu zilizokuwa zikitolewa ni kupunguziwa au kunyimwa posho. Hili bila shaka lilizorotesha afya za manamba waliokuwa wakifanya kazi ngumu.

Hata pale walipopata ajali hakukuwa na huduma stahili za afya kwa sababu mbalimbali kama vile umbali wa kituo cha afya na changamoto ya huduma ya kwanza. Inaelezwa katika riwaya teule kuwa katika siku za mwisho wa juma, manamba akipata ajali, hakukuwa na uwezekano wa kupelekwa hospitali mpaka Jumatatu asubuhi kama inavyofafanuliwa katika riwaya:

> Hapo shambani hapakuwa na huduma ya tiba ya aina yoyote; hata dawa ya vidonda tu ilikuwa hakuna ijapokuwa manamba wa kukata mkonge hujikata na mapanga yao hayo ya kazi na kuchomwa vibaya na miiba wakati wote humo kazini mwao (uk. 9).

Ingawa hakukuwa na vifaatiba, kazi ziliendelea kama kawaida. Kwa ujumla, manamba walifanya kazi katika mazingira hatarishi. Ili kukabiliana na changamoto hizo, manamba walitafuta njia mbalimbali za kujitibu pale walipopata ajali. Katika riwaya teule, inaelezwa kwamba baada ya Mzee Jabiri kupata ajali, Mnyapara Munubi aliamua kumganga kwa njia ambazo kwa hakika hazikuzingatia taratibu za kiafya:

> Kimya kimya Mnyapara Munubi akapiga magoti na kuzoa chini tope la udongo uliokuwa umelowa kwa mvua kubwa za usiku wa kuamkia siku hiyo na kuuchanganya na damu ya jeraha la Mzee Jabiri. Halafu akafinyangia hilo tope la udongo na damu kwenye jicho la Mzee Jabiri lililojeruhiwa na kuziba kabisa hilo tundu la kutisha. Kisha, kimyakimya hivyo hivyo, akang'oa jani la mkonge kutoka kwenye shina la hapo karibu na kuuma na kutoa kwa meno chane kubwa na kuanza kutafuna huo mkonge. ...Alipotafuna huo mkonge hadi kuulainisha kabisa kabisa, akautoa kinywani na kuubandika kwenye hilo tope alilozibia tundu la jichoni kwa Mzee Jabiri (uk. 8).

Msisitizo mkubwa wa dondoo hili ni kwamba matajiri wa Kizungu hawakujali afya za wafanyakazi wao hata kama walifanya kazi kwenye mazingira hatarishi. Sababu za kutokujali ni kuwaona manamba kama watu wa daraja la chini ambao

hawakustahili kupewa huduma kama binadamu wengine. Simulizi za watumwa zimesheheni visa vya afya zao kutokutiliwa maanani. Kwa mfano, Mary Prince anadai:

> *When we were ill, let our complaint be what it might, the only medicine given to us was a great bowl of hot salt water, with salt mixed with it, which made us very sick* (Prince, 1831).
>
> Tulipoumwa, hata tulalamike vipi, dawa pekee tuliyopewa ilikuwa bakuli kubwa la majichumvi ya moto yaliyochanganywa na chumvi, na kutufanya kuwa wagonjwa zaidi (Tafsiri yangu).

Suala la kujali afya halikuishia tu kukosa huduma katika siku za mwishoni mwa juma bali manamba walipoumwa na kushindwa kufanya kazi, hawakupewa ujira wa siku husika. Aidha, manamba aliyejeruhiwa au aliyepata ugonjwa ambao ungemfanya kukawia kurudi kazini, alipewa stahiki zake alizokwishazifanyia kazi na kufukuzwa bila kutibiwa. Kwa maneno mengine, manamba wa aina hiyo aliandaliwa kifo. Katika riwaya hii, kunaoneshwa pia ukatili wa matajiri wa Kizungu kwa manamba. Kwa mfano, inaelezwa mmiliki wa shamba, Tumbo Tumbo, alipokuwa akimpeleka Mzee Jabiri hospitalini, aliendesha gari kwa nguvu ili mgonjwa afariki dunia asiendelee kumgharimia. Hili lilitokea baada ya Mnyapara Munubi kushinikiza mgonjwa apelekwe hospitalini, yaani kutokumuunga mkono tajiri wake kwamba Mzee Jabiri apewe ujira wake akajiuguze mwenyewe. Matendo hayo, yanashabihiana na yale yanayosimuliwa katika simulizi za watumwa kuhusu huduma duni za afya. Simulizi hizo zinabainisha namna huduma za ukunga zilivyokuwa duni na kusababisha watoto au watumwa wanawake kufariki dunia. Kwa mfano, Harriet Jacobs anaeleza kuhusu Nancy ambaye alijifungua mtoto aliyefariki dunia muda mfupi baadaye. Hata hivyo, alirejea kazini kwenye mazingira magumu ndani ya majuma mawili.

Suala lingine ambalo linaelezwa kukiukwa katika maisha ya manamba ni kutoruhusu manamba kutembelewa na wake zao. Yumkini si katika mashamba yote, lakini kuna udokezi kuwa, katika mashamba mengi, waliishi wanaume peke yao. Hili liliwakosesha haki ya kingono na kindoa. Kukaa muda mrefu bila kukutana na wake zao, kuliathiri kwa kiasi kikubwa uzalianaji wa binadamu kwa sababu idadi kubwa ya wanaume waliondoka maeneo yao kama vile Nyanda za Juu Kusini na maeneo ya Tanganyika Magharibi, na kuishi miezi kadhaa katika maeneo ya uzalishaji, hususan Tanga na Morogoro.

### 5.2.7 Unyonyaji na Kazi za Kiimla

Sifa mojawapo kubwa ya utumwa ni mahusiano ya kinyonyaji baina ya mabwana na watumwa (Pargas, 2016). Mabwana hulenga kupata nguvukazi kwa gharama nafuu. Ndiyo maana wakoloni walianzisha kodi ili kuwapata vibarua. Inaelezwa kuwa hata hiyo kodi ilidaiwa zaidi wakati kulipohitajika vibarua wa kazi mashambani (Lwoga, 1987; Kangalawe, 2021). Ndiyo maana baadhi ya

wanazuoni huzitambua kazi hizi kama kazi za shuruti. Maana yake, manamba walitengenezewa mazingira ambayo yaliwalazimu kuwa manamba bila hiari yao.

Mfumo wa manamba umeandaliwa kwa misingi ya kinyonyaji ambapo manamba walishurutishwa kufanya kazi ili wapate kodi. Katika uainishaji wa sababu za kuingia utumwani au katika kazi za shuruti, van der Linden ameweka kazi za shuruti na utumwa katika kundi moja; na sababu mojawapo ya mtu kuingia utumwani ni ulipaji wa kodi ya fedha taslimu, mfumo uliowashinikiza waathirika wa mifumo hiyo ya kinyonyaji kuingia utumwani bila kupenda (van der Linden, 2016). Tofauti kubwa na utumwa wa hiari ambapo mtu anaamua kujiweka chini ya utumwa ili anufaike kwa chakula kwa mfano kama anavyoeleza van der Linden (2016), katika utumwa wa manamba mazingira ya kinyonyaji yameandaliwa kwa namna ambayo mtu wa kawaida hawezi kujinasua wala kubaini kwa urahisi kama anaingizwa utumwani kwa shuruti. Manamba walifanya kazi kwa ujira mdogo uliowawezesha kulipa kodi tu na kununua vitu vichache visivyo na tija kiuchumi kama inavyoelezwa katika riwaya ya *Miradi Bubu ya Wazalendo*:

> Mara kwa mara hao matajiri wa kigeni wa mkonge, kwa tamaa ya faida na kwa kutomwona mtu mweusi kuwa binadamu sawa na wao, waliwatumikisha manamba wao hadi wakafikia kikomo cha mtu kuweza kuvumilia na wakagoma. Lakini mara nyingi hiyo migomo ilivunjwa mara moja na kwa urahisi. Tajiri alikwenda Tanga au Morogoro au Dar es Salaam na kurudi anasindikizwa na askari wakiwa na bunduki na bakora na pingu, na viboko vikafikia kuimba, ... wenye kiburi wakapelekwa jela (uk. 16).

Dondoo hili linabainisha kuwa hakukuwa na fursa ya kudai haki na kufanya hivyo kulijibiwa na adhabu kali. Haya ni mazingira ya kitumwa kwa sababu njia pekee ya kumalizana na mfanyakazi asiyetimiza malengo ni kumwachisha kazi. Mazingira hayo ya kitumwa yanathibitishwa na matendo kama hayo waliyokumbana nayo watumwa kama vile Douglass (2005) anaposema kuwa mgomo wowote dhidi ya Mzungu ulisambaratishwa kwa adhabu ya kifo. Inaonekana mara baada ya kuingia katika manamba, si tu kwamba hakukuwa na uhuru wa kudai haki bali manamba hawakuruhusiwa kutoka hapo walipopangiwa na ilipotokea mmoja amekamatwa akitoroka, alipigwa viboko kama inavyofafanuliwa katika dondoo:

> Na siku hizo mtu akisha andikishwa manamba ya mkonge, zao kuu la biashara ya mkoloni wa Kiingereza Tanganyika, mpaka hapo manamba yake hiyo, ya miaka miwili au mitatu, au hata minne, itakapokwisha, huyo mtu alikuwa ni mfungwa wa huyo tajiri wa kigeni mwenye shamba la mkonge. ... na alikuwa hawezi kukanyaga nje ya shamba la bwana wake huyo bila idhini ya huyo tajiri (uk. 9).

Kwa hiyo, manamba walikuwa kifungoni. Sheria zilizoandaliwa ziliwafanya wawe watumwa katika kipindi chote cha umanamba wao. Simulizi karibu zote za

utumwa zinajadili kwa kina suala la unyonyaji na uhuru. Hakukuwa na tofauti kubwa baina ya utumwa (kama inavyosimuliwa katika simulizi za watumwa) na manamba katika kipindi cha ukoloni.

### 5.3 Utokaji katika Utumwa

Hatua ya mwisho ni uchambuzi wa mchakato wa kutoka katika utumwa. Kwa ujumla, kuna njia mbalimbali za kutoka katika utumwa kama zilivyopendekezwa na van der Linden (2016: 314). Miongoni mwa njia hizo ni kuondolewa na mwajiri, kuondolewa na mamlaka nyingine, kutoroka, na kifo. Katika riwaya teule, kuna njia kadhaa za kutoka utumwani au kazi za shuruti kama vile kuondolewa na mwajiri kwa sababu mbalimbali ikiwamo ugonjwa usiotibika haraka, kumaliza muda wa mkataba, kutoroka, na kifo. Kwa mfano, pale manamba alipoumwa ugonjwa au kuuguza jeraha ambalo lingetumia muda mrefu kupona, alifukuzwa ili akatibiwe nyumbani kwake kama inavyoelezwa katika riwaya teule:

> Manamba aliyeugua na kushindwa kwenda kazini ilikuwa siku hiyo halipwi, kwani hakujaza kipande chake. Na yule aliyeugua sana na ikaelekea hataweza kurudi kazini mapema, kwa kawaida alifukuzwa kazi (uk. 14).

Mfano huu unadhihirika zaidi baada ya Mzee Jabiri kujeruhiwa vibaya na kuwa na hali mbaya sana, mmiliki wa shamba, Tumbo Tumbo, anamwambia Mnyapara Munubi majeruhi apewe ujira wake kisha aende zake, "Fanya hesabu ya kipande yake, halafu lete ripoti ofisini. Talipa yeye halafu shauri kwisha" (uk. 14). Kutokana na hali mbaya aliyokuwa nayo Mzee Jabiri, yumkini pia kutokana na ukweli kuwa Mzee Jabiri na Mnyapara Munubi walikuwa wakitokea sehemu moja, Mnyapara Munubi alishauri majeruhi atibiwe.

Njia nyingine ya kutoka utumwani ni kumaliza mkataba wa kufanya kazi. Manamba walipotimiza mkataba wa kazi waliruhusiwa kuondoka. Hawakuwa na uamuzi mwingine wa kujiondokea pale walipotaka wao. Manamba hawakuwa na uwezo wa kusitisha mkataba. Kama inavyosisitizwa katika mfano uliotolewa katika sehemu ya 5.2.7. Inaelezwa kuwa katika maeneo mbalimbali matajiri huwa na hulka ya kurefusha mikataba ya watumwa wa aina hii kijanjajanja. Hata hivyo, hakuna ushahidi wa moja kwa moja katika riwaya teule zaidi ya tajiri Joji aliyekuwa na tabia ya kutoa adhabu inayofikia kufanya kazi kipindi kirefu bila malipo kama inavyoelezwa katika riwaya:

> Shambani kwa Kaburu Joji adhabu ya viboko ilikuwa haitolewi mara nyingi. Huyo tajiri wa kigeni adhabu ya viboko aliiona kama isiyo na faida kwake. Badala yake manamba aliyevunja sheria yake yoyote adhabu yake ya kawaida ilikuwa ni kufanya kazi mwezi mzima au zaidi bila kulipwa (uk. 26).

Yumkini, manamba ambaye hakulipwa mwezi mzima alipaswa kuongeza muda ili ajipatie japo ujira duni kwa ajili ya matumizi yake binafsi au kaya yake aliyoiacha kwa kipindi kirefu mbali nyumbani kwake.

Njia mojawapo ya kutoka manambani ilikuwa kutoroka. Baadhi ya manamba wasioridhishwa na huduma mbalimbali kutoka kwa matajiri wao, waliamua kutoroka. Walipotoroka waliamua ama kwenda zao makwao au kwenda kwa matajiri wengine wenye afadhali. Hili linadhihirishwa katika tukio ambapo Mnyapara Munubi na Saidi wanatoroka shambani kwa Tumbo Tumbo usiku mara baada ya kuutupa mwili wa Mzee Jabiri katika shimo la kinyesi. Mnyapara Munubi anasema:

> Hapa siyo mahali pa mtu kuishi tena, Umeshuhudia wewe mwenyewe jinsi huyu Mzungu alivyomwua baba yako, licha ya hayo mwanamke wa Kizungu hapo hospitalini kutaka kututukana akili zetu, kwa vile kwa Wazungu mtu mweusi ni nyani asiye na akili. Halafu sasa ona hii kufuru tunayotoka kufanya kwa amri yake! Funga mizigo yako tuondoke hapa (uk. 24).

Inaonekana utoro ulifanyika zaidi usiku kwa sababu manamba hakuruhusiwa kuondoka bila idhini ya tajiri wake.

Njia ya mwisho ya kutoka utumwani ilikuwa kifo kama inavyoelezwa katika riwaya kuwa Mzee Jabiri alifariki akipelekwa hospitalini kwa sababu gari liliendeshwa vibaya hali iliyosababisha kifo chake. Hii ndiyo ilikuwa hatima ya utumwa wake kwa Tumbo Tumbo. Kwa ujumla, manamba walitoka utumwani kwa namna mbalimbali ambapo hakukuwa na uhuru wa kujiamulia kutoka utumwani kwa hiari yao.

## 6.0 Hitimisho

Makala hii imechambua suala la utumwa katika kipindi cha ukoloni. Tofauti na mitazamo ya kihistoria kuwa utumwa ulikomeshwa na Waingereza, katika makala hii, suala la utumwa limechambuliwa kwa mtazamo mpana zaidi kwa kuchunguza vitendo vinavyoashiria utumwa. Kama ilivyodokezwa, utumwa ni hali ambayo inaweza kuwa ya muda mrefu au muda mfupi ambapo uhuru wa mwathiriwa huwekwa chini ya mtu mwingine kwa hiari au shuruti. Katika hali hiyo, mwathirika anapoteza uhuru wake wa kuchagua na kufanya anachotaka badala yake bwana wake humwamulia majukumu ya kutekeleza. Kwa mantiki hiyo, manamba walikuwa katika hali ya utumwa, na hakika walikuwa watumwa. Suala la utumwa lisiwekewe misingi yake katika kilongo cha kisiasa na kihistoria, badala yake vigezo vya uhusiano, uhuru na utumikishwaji vitumiwe ili kubaini sifa bainifu za utumwa.

Riwaya teule inaakisi kwa kiwango kikubwa hali iliyokuwapo wakati wa ukoloni wa Waingereza. Maudhui yake yamechangia kuweka historia ya Tanzania katika fasihi huku vipengele bainifu vya utumwa vikiwekwa bayana. Vipengele

hivyo vimelinganishwa na vile vinavyopatikana katika simulizi mbalimbali za watumwa. Simulizi hizi zimesaidia kubainisha sifa za utumwa ambazo ziliendelea kutamalaki hadi katika kipindi cha ukoloni Tanganyika. Kinachosikitisha zaidi ni kwamba mbari iliyoingizwa utumwani Amerika ndiyo iliyofanywa watumwa Afrika Mashariki chini ya Waarabu na baadaye Wazungu.

Kwa hiyo, ili kuepuka kupotosha historia, kuna haja ya kufafanua dhana nje ya wigo wa kisiasa kwa kuchunguza usahihi wake kwa kile inachokiwakilisha. Kufanya hivi kutarahisisha uchambuzi na uelewekaji wa matukio ya kihistoria na kuyalinganisha kwa usahihi zaidi kama ilivyobanishwa katika makala hii kuwa mfumo wa manamba ni aina mojawapo ya utumwa huku tofauti kubwa na utumwa mwingine ni kwamba huu ulikuwa utumwa wa muda si wa kudumu. Tofauti kubwa ni msamiati uliotumiwa ambapo, dhana ya manamba inaondoa dhana ya utumwa ambayo, kwa wengi, ina ukakasi kwa sababu ya historia yake mbaya duniani.

## Marejeleo


Adam, A.S. (2007). *Kasri ya Mwinyi Fuad*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.

Ajayi, J.F.A. (2002). “Unfinished Business: Confronting the Legacies of Slavery and Colonialism in Africa.” Wasilisho katika The Southern Asian Studies Regional Exchange Programme, Amsterdam. https://cssscal.org/pdf/publication/ade_ajayi.pdf.

Alembi, E. (2002). *The Construction of the Abanyole Perceptions on Death through Oral Funeral Poetry*. Helsinki: University of Helsinki.

Andrews, W.L. na Gates, H.L. (2007). *Slave Narratives. [William L. Andrews Selected the Contents and Wrote the Notes for this Volume.]*. 3. The Library of America 114. New York: Library of America.

Bamgbose, O. (2015). “The Cane, the Pain and the Punishment: Corporal Punishment in Perspective Society.” *The Lord Justice Journal: A Journal of the Law Students.* 6: 161-85.

Bibb, H. (2001). *The Life and Adventures of Henry Bibb: An American Slave*. C.J. Heglar (Mh.). Wisconsin Studies in Autobiography. Madison: University of Wisconsin Press.

Chinyere, A.C. (2024). “Crime and Punishment in African Indigenous Law.” Katika *Legalpedia*. https://legalpediaonline.com/african-indigenous-law/.

Douglass, F. (2005). *The Narrative of the Life of Frederick Douglass: An American Slave*. Webster’s German Thesaurus Edition. San Diego, CA: ICON Classics.

Deustch, J-G. (2006). *Emancipation Without Abolition in German East Africa, c. 1884-1914.* Oxford: James Currey.

Equiano, O. (1789). *The Interesting Narrative of the Life of Olaudah Equiano Written by Himself*. London.

Gross, E. na Stone, G.P. (1964). "Embarrassment and the Analysis of Role Requirements." *The American Journal of Sociology*. LXX (1): 1-15.

Hoy, W.G. (2013). *Do Funerals Matter? The Purposes and Practices of Death Rituals in Global Perspective*. New York, NY: Routledge.

Iliffe, J. (1979). *A Modern History of Tanganyika*. Cambridge: Cambridge University Press.

Jacobs, H.A. na Jacobs, J.S. (2000). *Incidents in the Life of a Slave Girl*. N. Painter (Mh.). Penguin Classics. New York: Penguin Books.

Kangalawe, H. (2021). "'Drinking Too Much, They Can't Work': The Settlers, the Hehe Work Discipline and Environmental Conservation in Mufindi, Tanzania, 1920-1960." *Tanzania Zamani.* XIII (1): 126-70.

Lane, P.J. (2021). "Slavery in Africa c. 500-1500 CE : Archaeological and Historical Perspectives." Katika C. Perry, D. Eltis, S.L. Engerman na D. Richardson (Wah.), *The Cambridge World History of Slavery*. Cambridge: Cambridge University Press. Kur. 531-52. https://doi.org/10.1017/9781139024723.022.

Lovejoy, P.E. (2000). *Transformations in Slavery: A History of Slavery in Africa*. Tol. 2. African Studies Series 36. Cambridge New York: Cambridge University Press.

Lwoga, C.M.F. (1987). "Historical Roots of The Labour Shortage Problem in the Sisal Industry in Tanzania: Contradictions of the Cheap Labour System". *Journal of Eastern African Research & Development.* 17: 18-33.

Mann, M. (1986) *The Sources of Social Power*. London: Cambridge University Press.

Mapalala, B. (1992). *Kwaheri Iselamagazi*. Tanzania Publishing House.

Mbilinyi, M. (1986). "Agribusiness and Casual Labor in Tanzania." *African Economic History*. 15: 107-141.

Mbiti, J.S. (1975). *Introduction to African Religion*. London: Heinemann.

Mbotela, J.J. (1959). *Uhuru wa Watumwa: The Freeing of the Slaves*. Nairobi: Nelson.

Muñoz-Valdivieso, S. (2020). "Slavery Fiction in Britain." *Journal of European Studies.* 50(2): 193-209. https://doi.org/10.1177/0047244120918481.

Murphy, L. (2012). *Metaphor and the Slave Trade in West African Literature*. Western African Studies. Athens, Ohio: Ohio University Press.

Nyanto, S.S. (2019). Slave Emancipation, Christian Communities and Dissent in Western Tanzania, 1878-1978. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Iowa.

Nyanto, S.S. na Becker, F.M. (2023). "In Pursuit of Freedom: Oaths, Slave Agency, and the Abolition of Slavery in Western Tanzania, 1905-1930". *Law and History Review*. 1-23. https://doi.org/10.1017/S0738248023000615.

Nyanto, S.S. (2024). *Slave Emancipation, Christian Communities and Dissent in Post-Abolition Tanzania, 1878-1978*. London and New York: James Currey.

Nyanto, S.S. na Becker F.M. (2025). "*Kijiji cha Watoro*: Resistance, Identity, and Social Life of Nyamwezi Runaway Slaves along the Central Caravan Route in Tanzania" *Slavery & Abolition*, 46(3): 567-586. https://doi.org/10.1080/0144039X.2025.2532901.

O'Rourke, T., Spitzberg, B.H. na Hannawa, A.F. (2011). "The Good Funeral: Toward an Understanding of Funeral Participation and Satisfaction." *Death Studies*. 35(8): 729-50. https://doi.org/10.1080/07481187.2011.553309.

Pargas, D.A. (2023). "Introduction: Historicizing and Spatializing Global Slavery." Katika D.A. Pargas na J. Schiel (Wah.), *The Palgrave Handbook of Global Slavery throughout History*. Cham: Springer International Publishing. Kur. 1-13. https://doi.org/10.1007/978-3-031-13260-5.

Pargas, D.A. (2016). "Slavery as a Global and Globalizing Phenomenon." *Journal of Global Slavery*. 1(1): 1-4. https://doi.org/10.1163/2405836X-00101004.

Prince, M. (1831). *The History of Mary Prince: A West Indian Slave*. London: F. Westley and A.H. Davis, Stationers' Hall Court na Waugh & Innes, Edinburgh. https://gutenberg.org/files/17851/17851-h/17851-h.htm.

Rodney, W. (1983). "Migrant Labour and the Colonial Economy." Katika W. Rodney, K. Tambila na L. Sago. *Migrant Labour in Tanzania During the Colonial Period: Case Studies of Recruitment and Conditions of Labour in the Sisal Industry*. Hamburg: Institut für Afrika-Kunde. Kur: 4-28.

Rossi, B. (2023). "Slavery in Francophone West Africa." Katika D.A. Pargas na J. Schiel (Wah.), *The Palgrave Handbook of Global Slavery throughout History*, 583-604. Cham: Springer International Publishing. https://doi.org/10.1007/978-3-031-13260-5_33.

Ruhumbika, G. (1995). *Miradi Bubu ya Wazalendo*. Dar es Saalam: Tanzania Publishing House.

Sabea, H. (2009). "The Limits of Law in the Mandated Territories: Becoming *Manamba* and the Struggles of Sisal Plantation Workers in Tanganyika." *African Studies*. 68(1): 135-61. https://doi.org/10.1080/00020180902827548.

———. (2010). "Codifying *Manamba* : History, Knowledge Production and Sisal Plantation Workers in Tanzania." *Journal of Historical Sociology*. 23(1): 144-70. https://doi.org/10.1111/j.1467-6443.2009.01362.x.

Semzaba, E. (1984). *Tendehogo*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Sharkey, W.F. (1992). "Use and Responses to Intentional Embarrassment." *Communication Studies*. 43(4): 257-75. https://doi.org/10.1080/10510979209368377.

———. (1993). "Who Embarrasses Whom?: Relational and Sex Differences in the Use of Intentional Embarrassment." Katika P.J. Kalbfleisch (Mh.),

*Interpersonal Communication: Evolving Interpersonal Relationships*. Hillsdale, NJ: LEA. Kur. 147-68.

Shimane, K. (2018). “Social Bonds with the Dead: How Funerals Transformed in the Twentieth and Twenty-First Centuries.” *Philosophical Transactions of the Royal Society B: Biological Sciences.* 373(1754): 20170274. https://doi.org/10.1098/rstb.2017.0274.

Taylor, Y. (1999). *I Was Born a Slave: An Anthology of Classic Slave Narratives*. The Library of Black America. Chicago (Ill.): Lawrence Hill Books.

van der Linden, M. (2010). “Unanticipated Consequences of ‘Humanitarian Intervention’: The British Campaign to Abolish the Slave Trade, 1807-1900.” *Theory and Society.* 39(3-4): 281-98. https://doi.org/10.1007/s11186-010-9106-4.

———. (2016). “Dissecting Coerced Labor.” Katika M.M. van der Linden na M.R. García (Wah.), *On Coerced Labor: Work and Compulsion after Chattel Slavery*. Leiden: BRILL. Kur. 293-322. https://doi.org/10.1163/9789004316386.

Vernet, T. (2013). “East Africa: Slave Migrations.” Katika I. Ness (Mh.), *The Encyclopedia of Global Human Migration*, 1st ed. Wiley. https://doi.org/10.1002/9781444351071.wbeghm188.

Williams, L.V. (1994). *The Representation of Slavery in Cuban Fiction*. Columbia: University of Missouri Press.

Wood, M. (2019). *The Black Butterfly: Brazilian Slavery and the Literary Imagination*. Morgantown: West Virginia University Press.